

Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 MEI, 2026 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2026.

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 01-10 MEI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilisababisha ukanda mvua kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani, na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo. Aidha, mifumo ya hali ya hewa iliyopo katika ukanda wa Ziwa Victoria pamoja na upepo wa bahari wenye unyevunuevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani viliimarisha zaidi mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 MEI, 2026.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea vipindi vifupi vya mvua kubwa zilizoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa Ziwa Viktoria.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2026.

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2026.

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhohofika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua kuendelea kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, nyanda za juu kaskazini mashariki na ukanda wa pwani, na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

Aidha, mifumo ya hali ya hewa iliyopo katika ukanda wa Ziwa Victoria kuimarika pamoja na upepo wa bahari wenye unyevunuevu uvumao kutoka mashariki na kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani vinatarajiwa kuendelea kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 MEI, 2026.

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara): Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Vipindi vya Mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua zinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): mvua nyepesi zinatarajiwa katika maeneo machache hususan yenye miinuko.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vya mvua nyepesi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na:

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz